# CALFONIA HILLS SECONDARY SCHOOL

**P. O. Box 10777, Mwanza Tanzania**

**Email: info@calfoniahills.ac.tz**

**Mobile: +255 767 307 367 +255 747 645 513**

**Website: www.calfoniahills.ac.tz**


# JOINING INSTRUCTIONS

## MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI CALFONIA HILLS KWA MWAKA WA MASOMO – 2025.

## UTANGULIZI

Shule ya Sekondari Calfonia Hills ni shule ya binafsi ya bweni na kutwa. Shule ni ya mchanganyiko inayoendeshwa na Walimu mahiri wanaotoa elimu bora.

### MAHALI SHULE ILIPO

Shule ya Sekondari **Calfonia Hills** ipo **Nyegezi – Majengo,** kilometa 2 kutoka **Stendi ya Mabasi Nyegezi**, Shule ina eneo la kutosha na mazingira tulivu ya kujifunzia.

### KAULI MBIU YA SHULE

***NGAZI YA MAFANIKIO (STEPS TO SUCCESS)***

### UTARATIBU WA MALIPO YA ADA YA SHULE KWA MWAKA WA MASOMO 2024.

| MWEZI | KUTWA | | | | BWENI | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Form I | Form II | Form III | Form IV | Form I | Form II | Form III | Form IV |
| January | 300,000 | — | 300,000 | - | 450,000 | 450,000 | 450,000 | 600,000 |
| April | 300,000 | — | 300,000 | - | 450,000 | 450,000 | 450,000 | 600,000 |
| July | 300,000 | — | 300,000 | - | 450,000 | 450,000 | 450,000 | 600,000 |
| September | 300,000 | — | 300,000 | - | 450,000 | 450,000 | 450,000 | |
| JUMLA | 1,200,00 | — | 1,200,000 | - | 1,800,000 | 1,800,000 | 1,800,000 | 1,800,000 |

### MALIPO YA MICHANGO MBALIMBALI

| Aina ya michango | Kidato cha I | Kidato cha II | Kidato cha III | Kidato cha IV | |
|---|---|---|---|---|---|
| Taaluma (ada ya mitihani wa taifa) | | 100,000 | | 200,000 | |
| Sare ya shule | | | | | 180,000 |
| Usajili na kitambulisho | | | | | 20,000 |
| Mahafali | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 100,000 | |
| June & December program | 100,000 | 100,000 | 100,000 | 100,000 | |
| Ziara ya kitaaluma | | | | 100,000 | |

 Ada ya shule kwa mwanafunzi wa bweni ni sh **1,800,000/=** na kwa mwanafunzi wa kutwa ni **sh 1,200,000/=**

- Ada inaweza kulipwa yote kwa mara moja ama kwa awamu **nne kwa kidato cha kwanza hadi cha tatu na kwa kidato cha nne wanatakiwa kulipa awamu tatu tu kwa wanafunzi wa kutwa na bweni** kama ilivyoainishwa katika jedwali hapo juu, pia ada inaweza kulipwa kwa awamu mbili.

Malipo ya ada ya shule na ada ya mtihani y apitie benki ya **NMB** au benki ya posta **(TPB)**

**All payments must be affected through (Malipo yote yafanyike kupitia NMB au TPB)**

**1. NMB BANK**

Name of account (jina la Akaunti): **CALFONIA HILLS SECONDARY SCHOOL** Account Number (Namba ya Akaunti) **32910000048**

**2. TPB BANK**

Name of account (jina la Akaunti) **CALFONIA HILLS SECONDARY SCHOOL** Account Number (Namba ya Akaunti) **280204000121**

**MUHIMU:** *Andika jina kamili la mwanafunzi wakati wa kufanya malipo.*

**HATUPOKEI FEDHA TASLIMU. LETA RISITI YA BENKI**

# MAHITAJI YA SHULE

**WAKATI WA KURIPOTI SHULENI**

Mwanafunzi aje na vitu vifuatavyo: - 1. **Risiti ya Benki** ya malipo ya ada.

2. **Fomu ya maombi** iliyojazwa kikamilifu.
3. Picha **2 za passport** zilizopigwa hivi karibuni.
4. **Nakala ya cheti cha kuzaliwa.**
5. **Picha ya mzazi /mlezi (passport size)** 6. **Uthibitisho wa vipimo vya hospitali kiafya. (Medical report form)** 7. **A4** Karatasi nyeupe **Rimu nne (4) (double A) kwa mwaka**
8. **Mafaili (Spring files) matano (**5) matatu kwa matumizi ya shule na mawili kwa matumizi ya mwanafunzi.
9. **Graph pads 2 kwa ajili ya shule**
10. **Vikombe vya plastiki viwili (2) (nusu lita kila kimoja)**.
11. **Container ya plastiki yenye vyumba na kijiko** kwa ajili ya chakula.

**MAHITAJI YA DARASANI**

1. Begi jeusi la kubebea madaftari. Haturuhusu mwanafunzi kubeba madaftari mikononi
2. Bofa (mathematical set).
3. Madaftari (Counter books) 16 na yaandikwe majina vizuri.
4. Rula ndefu (sentimeta 30).

5. Kalamu za wino na penseli za kutosha.

6. Majaladio ya madaftari (rangi ya khaki).
7. Madaftali ya graph 2 kwa matumizi ya mwanafunzi
8. Kamusi ya Kiswahili (TUKI).
9. English Dictionary (Oxford)
10. Four figure kwa kidato cha tatu.
11. Saa ya mkononi (isiwe kubwa saana wala yenye mapambo).

**SARE YA SHULE**

1. Sare ya shule ni sketi/suruali, shati, tai, sweta, T-shirt, track suit na sare ya bweni. Gharama yake **sh. 180,000/=**
2. Viatu vyeusi vya mfuto (visivyo na visigino virefu (flat shoes) na viwe vya kamba
3. Mkanda mweusi wa suruali (usiwe mpana wala wenye chuma kikubwa au urembo) wa ngozi kwa wavulana.

**WANAFUNZI WA BWENI**

Wanafunzi wa BWENI wanatakiwa kuja na vitu vifuatavyo:

1. Godolo size: futi $2^1/_2$ kwa futi 6
2. Shuka 2: rangi ya pinki(andika majina kwa kudarizi)
3. Mto (1), blanketi (1), taulo (1). 4. Nguo za ndani 1 dozen (12)
5. Vest 3 nyeupe kwa wavulana
6. Spices 3 nyeupe kwa wasichana
7. Pads kwa wasichana (za kutosha)
8. Night dress 2 kwa wasichana
9. Khanga au vitenge 2 kwa wasichana.
10. Raba nyeupe kwa ajili ya michezo
11. Ndala aina ya bata tu
12. Chandarua (rangi ya blue)
13. Ndoo mbili za ujazo wa lita 10 kila moja 13. Sanduku la chuma la rangi ya bluu lenye kufuli.
14. Dawa ya meno na mswaki.
15. Mafuta ya kupaka, meupe yasiyo na harufu ya kuvutia haturuhusu lotion wala cream
16. Sabuni nyeupe (miche mitatu)
17. Kiwi nyeusi na brashi yake
18. Seti ya Kitana wembe na packet mbili za nyembe 19. Dodoki la kuogea na kikombe cha plastic cha kuogea.
20. Kitambaa cha mkononi rangi yoyote.
21. Pesa ya matumizi ikabithiwe kwa mhasibu wa shule (mwanafunzi haruhusiwi kumiliki fedha)
22. Kama mwanafunzi ana kadi ya bima ya matibabu aje nayo na ikabidhiwe kwa atakayekuwa anawapokea wanafunzi.
23. Mwanafunzi mwenye matatizo ya kiafya lazima **AFIKE NA BARUA YA DAKTARI** na awe makini kuwakumbusha walimu kuhusu tatizo lake.

**Wazazi/walezi wanaotambulika na shule tu**, wanaweza kuwatembelea wanafunzi shuleni kila jumapili ya mwisho wa mwezi kama itakavyoelekezwa.
**Wazazi/walezi hawaruhusiwi kuja na chakula siku ya kutembelea wanafunzi**. Haturuhusu mtu mwingine asiyetambulika na shule kuja kumtembelea mwanafunzi.

## SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE

### UTANGULIZI:

Kuanzia unapojiunga na Shule ya Sekondari Calfonia Hills hadi unapohitimu, elimu na ustawi wako ni jukumu letu. Ili kufikia lengo hili, kila mwanafunzi ni muhimu akazingatia taratibu na sheria za shule kama zilivyoainishwa hapo chini.

### ZIFUATAZO NI SHERIA ZA SHULE:

1. Wanafunzi wote wanapaswa kuripoti siku ya kufungua shule saa moja na nusu asubuhi.
2. Kila mwanafunzi anatakiwa kuishi kwa heshima na watu wote bila kujali umri, jinsia, rangi au dini.
3. Mwanafunzi **haruhusiwi** kubadili dini bila idhini ya wazazi wake.
4. Shule haitachukua dhamana kwa mwanafunzi atakayepata madhara au kuumia nje ya shule akiwa ametoroka.
5. Shule itafungwa mara utokeapo ugonjwa wa mlipuko.
6. Ndugu au jamaa hawapaswi kuwatembelea wanafunzi wakati wa masomo. Kama kuna dharura mhusika afike ofisi ya utawala.
7. Wanafunzi hawaruhusiwi kufika maeneo yafuatayo isipokuwa kwa ruhusa maalumu.
   (i) Ofisi ya walimu.
   (ii) Vyoo vya jinsia nyingine.
   (iii) Nyumba za wafanyakazi wa shule.
   (iv) Maabara.
   (v) Jiko la Shule.
8. Kila mwanafunzi anapaswa kushiriki shughuli za nje ya darasa kulingana na ratiba ya shule.
9. Nywele za wanafunzi wote (wavulana na wasichana) ziwe fupi wakati wote bila mitindo ya aina yoyote. Si ruhusa kujiremba kwa aina yoyote ukiwa Mwanafunzi wa shule ya Sekondari Calfonia Hills.
10. Wageni wote wanatakiwa kufikia ofisi ya utawala kabla ya kuwasiliana na mwanafunzi yeyote.
11. Mwanafunzi haruhusiwa kutumia dawa aina yoyote bila taarifa kwa uongozi. Ukiwa na dawa wasiliana na mwalimu mara moja.
12. Mwanafunzi hataruhusiwa kuingia darasani bila kulipa karo ya shule.
13. Sare ya shule iheshimiwe na itanunuliwa kutoka shuleni tu. Hairuhusiwi **kupunguza** au **kubadili** sare ya shule kwa namna yoyote ile.
14. Ni marufuku kumsalimia mtu mzima **bila kusimama au kutomsalimia kabisa.**
15. Hairuhusiwi kuacha kwa makusudi kupokea wageni au mfanyakazi wa shule anapokuwa na mzigo uwapo nje ya darasa.
16. Ruhusa zote za wanafunzi kutoka nje ya shule zitatolewa na Mkuu wa Shule au Msaidizi wake tu.
17. Mahusiano kwa wanafunzi wote ni kaka na dada na si vinginevyo.
18. Hairuhusiwi kutumia aina zote za vileo.
19. Si ruhusa kutembelea kumbi za starehe, matamasha ya starehe au fukwe kwa lengo la starehe ukiwa mwanafunzi wa shule ya Sekondari Calfonia Hills hata wakati wa likizo.
20. Si ruhusa Kumiliki simu, vifaa vya muziki, kamera, picha zisizo na maadili na sitaha.
21. Njia ya kutatua migogoro au tatizo kwa kila mwanafunzi ni kufuata taratibu sahihi na si vinginevyo.

22. Mwanafunzi aliye simamishwa shule haruhusiwi kuonekana eneo la shule.
23. Mwanafunzi haruhusiwi kuambatana na mwanafunzi aliyesimamishwa au kufukuzwa shule ndani ya eneo la shule.
24. Utoro wa aina yoyote haukubaliki shuleni Calfonia Hills.
25. Mazingira ya shule sharti yatunzwe katika hali ya usafi.
26. Ubaguzi wa aina yoyote hauruhusiwi shuleni hata kidogo.
27. Wakati wa kufunga shule kila mwanafunzi ataondoka shuleni akiambatana na mzazi.

## MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

(i) Kumiliki na kutumia madawa ya kulevya.
(ii) Mahusiano ya kimapenzi.
(iii) Kuhusika katika kuwatafutia wanafunzi wengine marafiki wa kimapenzi.
(iv) Wizi wa aina yoyote.
(v) Udhalilishaji wa aina yoyote.
(vi) Kuondoka maeneo ya shule bila ruhusa ya maandishi.
(vii) Kupata au kusababisha ujauzito.
(viii) Kutoa au kushiriki katika utoaji mimba.
(ix) Ulevi wa aina yoyote.
(x) Kupatikana na hatia mahakamani.
(xi) Kupigana / kupiga pamoja na makosa mengine ya jinai.
(xii) Kugomea adhabu halali kwa makusudi.
(xiii) Kuchochea au kushiriki kwenye mgomo au vurugu.
(xiv) Kuoa au kuolewa.
(xv) Kulala wanafunzi wawili kitanda kimoja au kutumia shuka/blanketi la mwanafunzi mwingine.
(xvi) Kutohudhuria masomo bila taaarifa shuleni kwa zaidi ya siku sabini na tano ***(75)***. Hii ni kwa mujibu wa sheria ya Elimu ***Na. EDC.43/60 ya 23/5/1994 ibara ya 4 (2).***
(xvii) Kuonekana eneo la shule baada ya kusimamishwa shule.

## MAKOSA YATAKAYOSABABISHA KUSIMAMISHWA SHULE

(i) Uzururaji wakati wa masomo.
(ii) Utoro wa aina yoyote.
(iii) Kumiliki simu, vifaa vya muziki, Kamera na silaha. (iv) Kuandika ukutani au mahali popote kwenye jengo.
(v) Kujiremba kwa aina yoyote kama vile kuvaa hereni, bangili, kofia n.k.
(vi) Kuvaliana nguo, viatu, ndala au soksi.
(vii) Kuchangia au Kutumia kwa makusudi ndoo au chombo cha kuogea cha mwanafunzi mwingine.
(viii) Matumizi mabaya ya ruhusa ya kutoka nje.
(ix) Kubadili sare ya shule au kupunguza sare kinyume na taratibu zinazokubalika.
(x) Kuonekana pamoja na mwanafunzi aliye fukuzwa au kusimamishwa shule katika eneo la shule na penginepo.
(xi) Kutofuata utaratibu katika kutatua matatizo binafsi, ya darasa au ya jamii kwa ujumla.
(xii) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma, picha za viongozi wa chama/serikali na Bendera ya Taifa. Mhusika pia atafidia uharibifu uliofanyika.
(xiii) Kudharau Wimbo wa Taifa, wimbo wa shule, Tanzania-Tanzania na Tazama Ramani.

(xiv) Kuonekana katika kumbi za starehe, matamasha ya starehe au fukwe kinyume na taratibu halisi.

(xv) Kuondoka shuleni bila idhini ya mzazi na shule wakati wa kufunga shule.

## UTARATIBU WA MITIHANI

(i) Udanganyifu wa aina yoyote katika mitihani ukitokea adhabu yake ni kufutiwa matokeo kwa masomo yote. Mwanafunzi atakayehusika na udanganyifu kwenye mitihani atasimamishwa masomo au kufukuzwa shule mara moja.

(ii) Baada ya mitihani wanafunzi wataendelea na utaratibu wa shule kama kawaida.

(iii) Wanafunzi wazingatie na kufuata taratibu za mitihani aina yote.

(iv) Maksi za chini kwa somo la Hisabati ni 30%.

(v) Kabla ya kujiunga na shule mwanafunzi atapewa mtihani wa kumpima.

(vi) Akishindwa kufikisha wastani wa maksi 45% hatapokelewa.

**NB:** *Uvunjaji wa sheria au taratibu za shule unaweza kusababisha kusimamishwa masomo au kufukuzwa shule mara moja.*

## SHERIA ZA BWENII

1. Usafi wa kila siku ni lazima kwa kila mwanafunzi wa bweni. Hii ni pamoja na kuoga, kufua nguo, kufagia, kufuta vumbi na kutandika kitanda chake.
2. Mwanafunzi hatakiwi kuonekana bwenini muda wa vipindi ila kwa ruhusa maalum. Hii ni kwa wakati wa masomo ya kawaida, pamoja na preps (wakati wa kujisomea)
3. Wanafunzi wa kutwa na wageni wengine hawaruhusiwi kuingia bwenini.
4. Mgeni kumwona mwanafunzi wa bweni lazima apate kibali toka ofisi ya utawala.
5. Upishi wa aina yoyote ile hauruhusiwi shuleni. Hivyo mwanafunzi haruhusiwi kuleta wala kuonekana akiwa na kifaa chochote kinachosadikiwa kuwa kinaweza kutumika kupika kitu chochote.
6. Mwanafunzi hatakiwi kuleta chombo chochote cha umeme bwenini.
7. Kuhudhuria masomo ya kujiandaa (prep) jioni ni lazima kwa kila mwanafunzi. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria masomo jioni kila siku.
8. Ni marufuku kununua na kuleta vyakula vya aina yoyote bwenini kutoka nje ya shule.
9. **Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na fedha Bwenini**. Pesa yote ikabidhiwe ofisini wakati wa kuripoti na itumiwe vizuri inapohitajika. Ni makosa mwanafunzi kuanzisha au kuendesha mikopo shuleni.

**ZINGATIA YOTE YALIYOAINISHWA HAPO JUU.**

**Kumbuka: Bidii yako katika TAALUMA na NIDHAMU ndiyo njia ya mafanikio.**

Karibu Sana

____________ Tarehe ___________

Mussa Lugoye.
MKUU WA SHULE

# CALFONIA HILLS SECONDARY SCHOOL

**P. O. Box 10777, Mwanza Tanzania**

**Email: info@calfoniahills.ac.tz**

**Mobile: +255 767 307 367 +255 747 645 513**

**Website: www.calfoniahills.ac.tz**


Applicant photo

Picha ya muombaji

**UTANGULIZI**

**Shule ya Sekondari Calfonia Hills** iliopo **Nyegezi - Majengo Mapya** wilaya ya **Nyamagana**, jijini **Mwanza** kilometa 2 kutoka **Standi ya Mabasi Nyegezi**. Ni shule ya mchanganyiko bweni na kutwa. Wanafunzi wote wa Kidato cha Pili na Nne ni wa bweni. **Tunatoa elimu na malezi bora kwa wote.** Shule itafunguliwa tarehe 13/01/2025

**Applicant's details (Taarifa za Mwombaji)**

Full Name (Jina Kamili) ..........................................................................................................

Sex (Jinsia) ........................................

Class (Kidato)....................................

Date of birth (Tarehe ya kuzaliwa)...............................................District of Birth (Wilaya ulipozaliwa) ...............................................Religion (Dini yako) .............................................

Race/Tribe (Kabila).................................Nationality (Utaifa).................................................

Physical Address (Mahali Unapoishi) (Street/Village/Mtaa/Kijiji) ........................................

(Ward/Kata).........................District/Wilaya.........................Region/Mkoa..........................

Occupation of parent/ Guardian (Kazi ya mzazi/mlezi .....................................................

Parent's/Guardian's Phone Number (Simu ya Mzazi/Mlezi)

.........................................................................., ...................................................................

**For parent/guardian (kwa Mzazi/Mlezi)**

Does your child suffer any chronic illness? (Yes/No) if yes specify the illness (je mtoto wako anayo matatizo ya kiafya? Kama ndiyo tafadhali eleza)

____________________________________________________________

*(Onyesha cheti cha daktari wakati wa kuripoti iwapo mwanao ana tatizo la afya.)*

**ACADEMIC RECORDS (TAARIFA ZA KITAALUMA)**

Schools attended and highest class reached in each school (shule ulikosomea na darasa la juu ulilofika kila shule)

| **Name of school attended ulikosomea)** | **Highest class reached (darasa la juu ulilofika)** | **Year (Mwaka) (shule** |
|---|---|---|

1. Shule ya Msingi    Namba ya Mtihani Darasa la Saba    Mwaka uliomaliza

   ______________________________ ______________________________    ____________

2. Shule Uliyochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza

   ______________________________________________________________

3. Shule ya Sekondari unaposoma    PREM No.

   ______________________________    ____________________

4. Shule ya Sekondari  Namba ya mtihani Kidato cha Pili    Mwaka uliomaliza

   ____________ ______________________________    ____________

5. Namba ya simu ya mkuu wa shule ______________________________

**DATE OF EXAMINATION (TAREHE YA MTIHANI)**

The entrance examination will be held when you submit this form to school or scheduled to later dates. (Mtihani wa kujiunga utafanyika utakaporudisha fomu hii au unaweza kupangiwa siku ya kufanya mtihani).

Kwa **Kidato cha Kwanza 2025 na wahamiaji** mitihani ya kujiunga inafanyika hapa shuleni,

**Application Fee (Ada ya Maombi):**

You are required to pay **Tsh 20,000/=** (Non-refundable)  Tafadhali lipia **Tsh 20,000/=** kama ada ya maombi(Pesa hii haitarudishwa) baada ya kulipia

CALTONIA HILLS SECONDARY SCHOOL (CHSS) STEPS TO SUCCESS

**UTARATIBU WA MALIPO YA ADA YA SHULE**

| MWEZI | KUTWA | | | | BWENI | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Form I | Form II | Form III | Form IV | Form I | Form II | Form III | Form IV |
| January | 300,000 | __ | 300,000 | __ | 450,000 | 450,000 | 450,000 | 600,000 |
| April | 300,000 | __ | 300,000 | __ | 450,000 | 450,000 | 450,000 | 600,000 |
| July | 300,000 | __ | 300,000 | __ | 450,000 | 450,000 | 450,000 | 600,000 |
| September | 300,000 | __ | 300,000 | __ | 450,000 | 450,000 | 450,000 | |
| JUMLA | 1,200,00 | __ | 1,200,000 | __ | 1,800,000 | 1,800,000 | 1,800,000 | 1,800,000 |

- Ada inaweza kulipwa yote kwa mara moja ama kwa awamu **nne kwa wanafunzi wa kutwa na bweni** kama ilivyoainishwa katika jedwali hapo juu.
- Malipo ya michango yote yalipwe mwanzo wa mwaka.
- Wazazi watakaoingia utaratibu wa makubaliano na shule wataweza kulipia kwa awamu 10

**All payments must be affected through (Malipo yote yafanyike kupitia NMB au TPB)**

**1.NMB BANK**

Name of account (jina la Akaunti): **CALFONIA HILLS SECONDARY SCHOOL** Account Number (Namba ya Akaunti) **32910000048**

**2. TPB BANK**

Name of account (jina la Akaunti) **CALFONIA HILLS SECONDARY SCHOOL** Account Number (Namba ya Akaunti) **280204000121**

**MUHIMU:** *Andika jina kamili la mwanafunzi wakati wa kufanya malipo.*

**For Official Use Only**

Selected _______________ **NOT** Selected because ______________________________________

Reg. No.__________________

Checked and authorized for admission by (Name) ____________________________________

Designation ____________________ Signature __________________ Date ____________________

**Welcome to Calfonia Hills Secondary School**

_____________

Mussa Lugoye

**Headmaster** Date _______________

**MEDICAL INFORMATION/ TAARIFA YA HOSPITAL**

To be completed by medical officer from a recognized Government Hospital.

Full Name of Student ____________________________________________

Sex: male/female ______________________

Blood count (Red and White) ______________________________________

Stool examinations: _______________________________________________

T.B :_________________________ Skin: ____________________________

Eye test: ______________________ Ears: ____________________________

Chest: _______________________ Spleen: __________________________

Abdomen: _____________________________________________________

**ADDITIONAL INFORMATION**

E.g. Physical defects/impairment pediatric disorders: ______________________

I certify that the above is fit/unfit to pursue studies as stated above.

Signature: _______________________________________________

_______________________________________________________ **MEDICAL OFFICER**

DATE:________________________________________

Rubber Stamp

**NOTE**: STUDENT SHOULD SEND OR BRING THE COMPLETED FORM TO SCHOOL TOGETHER.

CALLONIA HILLS SECONDARY SCHOOL (CHSS) STEPS TO SUCCESS